



# Hadithi ya Sungura na Mbwa



Hapo kale, sungura na mbwa walikuwa marafiki. Walikuza mazao mengi. Walikuza ndizi, mahindi, maharagwe na mihogo.



Sungura alipewa kazi ya kulima.  
Mbwa naye alichunga mimea. Wote  
wawili walifanya kazi kwa bidii.



Siku moja ndovu alivamia shamba. Ndovu alianza kuharibu mazao. Sungura alipiga kelele. Mbwa alisikia kelele. Mbwa aliwaita mbwa wenzake.

Walienda pamoja hadi shambani.  
Walimfukuza ndovu. Waliokoa mazao.  
Sungura alimshukuru mbwa.



## Maswali

1. Sungura alipewa kazi gani?
2. Sungura na mbwa walikuza aina ngapi za mazao?